

HANA SALAMA MSHONGO

1. Huba leo kwa mpango, na tena zina kiwango,
Ama wa nyonda ulingo, ni mtungu kama nyongo,
Aula hiyo mifungo, kwa waliovunja ungo,
Hana salama mshongo, asipojekea kingo.
2. Kuno kukata maungo, matembezi ya maringo,
Bora kuyapa mgongo, hayawi ila ni ongo,
Kila mshika matango, natija yake ukongo,
Hana salama mshongo, asipojekeya kingo.
3. Ndwele isopata fingo, ya vitisho na uzingo,
Ipete msongombwingo, ikamkoroga chango,
Si mjuzi ni msungo, matoni yuna matongo,
Hana salama mshongo, asipojekea kingo.
4. Mkwere mtu mrongo, akusudiapo lengo,
Aziamilipo kengo, akilunga miviringo,
Alivyotokeza bungo, mche au ule mango,
Hana salama mshongo, asipojekeya kingo.
5. Mwenendo wa songosongo, zama za sasa mzingo,
Zina iwile tinyango, uroda wazuga bongo,
Muwi hupijiwa kongo! dauni ana utango,
Hana salama mshongo, asipojekeya kingo.
6. Toto shoo na purungo, latetemesha viungo,
Lilivyojipiga gongo, utake chake kitengo,
Asaa ni kikaango, cha kukupokeza jongo,
Hana salama mshongo, asipojekeya kingo.
7. Wazinifu milolongo, wakufanzile kibyongo,
Si kitu maji ya shingo, ni uziwa wa vibwengo,
Hukwisha uwe ngongongo, khatima waliya nongo,
Hana salama mshongo, asipojekeya kingo.
8. Hawara mwana ushongo, uzinzi kushika mwengo,
Hana raha ni mafyongo, walia dhiki ja ng'ongo,
Atenda kutaka mbango, akakwatiya michango,
Hana salama mshongo, asipojekeya kingo.
9. Tamati penye ukingo, nakhitimisha utungo,
Mume lidumishe jengo, na mke siwate pengo,
Wele wavunda mlango, wafao hawana wango,
Hana salama mshongo, asipojekeya kingo.

Omar Babu "Abu Marjan"
Chuo Kikuu cha Ohio State
Columbus, Ohio, Marekani
